# JARIDA MAALUM

# DIPLOMASIA YA UCHUMI




TOLEO LA 01 MWEZI MARCH, 2023



# TANZANIA NA DENMARK KUKABILIANA NA MABADILIKO YA TABIANCHI

Waziri wa Fedha na Mipango Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, amesema kuwa Dermark imekubali kushirikiana na Tanzania katika kupambana na mabadiliko ya tabianchi ambayo yamekua yakiathiri shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Dkt. Nchemba ameyasema hayo Doha nchini Qatar baada ya kukutana na kufanya mazungumzo na Waziri wa Ushirikiano wa Maendeleo na Sera za Mabadiliko ya Tabianchi wa Serikali ya Kifalme ya Denmark, Mhe. Dan Jorgesen, wakati wa Mkutano wa Tano wa Umoja wa Mataifa wa nchi zinazoendelea za kipato cha chini.

Alisema nchi hizo mbili zimekubaliana kuzielekeza Taasisi zao kuendelea kushirikiana katika Nyanja mbalimbali hususani kukabiliana na mabadiliko hayo ya tabia nchi ili kukuza uchumi.

"Licha ya makubaliano yaliyofikiwa katika mkutano huu, tumekua na ushirikiano mzuri na Dernmark ambapo Serikali yetu hupokea fedha nyingi kupitia Taasisi za Denmark ambazo hutumika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo", alisema Dkt. Nchemba.

Alisema kuwa mkutano kati ya nchi hizo mbili ni muendelezo wa mikutano mbalimbali ambayo imekuwa ikifanyika hivyo mazungumzo ya sasa ni jitihada za kuendelea kuimarisha ushirikiano huo wa maendeleo katika sekta mbalimbali za maendeleo.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Zanzibar, Mhe. Saada Mkuya, amesema kuwa Serikali ya Zanzibar imepata manufaa makubwa katika sekta za kijamii katika sekta ya afya, elimu na miundombinu.

Alisema Zanzibar na Tanzania kwa ujumla imeweka mikakati kabambe ya kuhakikisha inatekeleza diplomasia ya kiuchumi na nchi mbalimbali ili kuvutia uwekezaji na kuwaletea wananchi maendeleo, hivyo mikutano inayoendelea na nchi nyingine ni miongoni mwa jitihada za kufanikisha adhma hiyo.

Kwa upande wake Waziri wa Ushirikiano wa Maendeleo na Sera za Mabadiliko ya Tabianchi wa Serikali ya Kifalme ya Denmark, Mhe. Dan Jorgesen, ameipongeza Serikali ya Tanzania kwa kuendeleza ushirikiano kati ya nchi hizo.

Mhe. Jorgesen amesema kuwa pamoja na upya wa Serikali yake iliyopo madarakani baada ya uchaguzi mkuu wa Novemba 2022 Serikali ya mseto ya Denmark itaendelea kuimarisha ushirikiano na Tanzania katika nyanja mbalimbali.

“Mabadiliko ya Tabianchi ni masuala ambayo yanapaswa kupewa kipaumbele na kila mmoja wetu kutokana na athari zinazoendelea kujitokeza kutoka na changamoto hiyo”, alisema Mhe. Jorgesen.

Aidha, Mheshimiwa Jorgesen amesema Serikali yake inayoongozwa na Waziri Mkuu Mhe. Mette Frederiksen, anao ufahamu mkubwa kuhusu siasa za Bara la Afrika hivyo itasaidia kuongeza ushirikiano kati ya Denmark na Tanzania.



# WANAWAKE WIZARA YA FEDHA WATOA MSAADA SHULE YA MSINGI BUIGIRI

Watumishi Wanawake Wizara ya Fedha na Mipango wametoa msaada wa mahitaji ya msingi kwa wanafunzi wenye ulemavu wa ngozi na wasioona ili kuwawezesha kukidhi mahitaji yao.

Wametoa msaada huo walipotembelea Shule ya Msingi Buigiri iliyopo Wilaya ya Chamwino, yenye Watoto wenye mahitaji maalumu ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya siku ya wanawake duniani ambayo huadhimishwa kila ifikapo Machi 8.

Ziara hiyo iliongozwa na Afisa Utawala Wizara ya Fedha na Mipango Bi. Irene Kipwate ambaye alieleza kuwa watumishi wanawake wa Wizara wameguswa na Watoto hao na kuona umuhimu wa kuwatembelea hasa katika maadhimisho ya siku ya wanawake duniani ili kuzungumza nao na kuwapatia msaada huo.

''Tumekuja kwa niaba ya Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, kuwaona na kuwapatia zawadi tulizokuja nazo, kama mama tumefarijika kuwatembelea watoto hawa ambao kwa umri huu mdogo walipaswa kuwa na wazazi wao lakini kutokana na changamoto za kiafya wako hapa hivyo tunawapongeza walimu na walezi kwa kazi nzuri mnayoifanya kwani Watoto wana afya njema'', alisema Bi. Kipwate.

Alisema kama wazazi wanatamani kuona Watoto hao wakifikia ndoto zao hivyo kwa nafasi yao wataendelea kuwatembelea na kutoa misaada kwa kadiri watakavyoweza.

Aidha, alitoa wito kwa wanawake na wananchi kwa ujumla wajitoe kusaidia Watoto hao kwani wana mahitaji mengi hivyo wakumbuke kituo hicho licha ya Serikali na Kanisa kuhudumia kituo hicho na vingine, wananchi waguswe kuwaona Watoto hao na kuwapatia misaada mbalimbali.

Naye Mwenyekiti wa kamati ya wanawake Wizara ya Fedha na Mipango Bi. Joyce Pallangyo, ameshukuru uongozi wa shule hiyo kwa kuwapokea na kuwashukuru waalimu na walezi wa shule hiyo kwa huduma wanayotoa kwa Watoto hao na kuwaombea baraka kwa kazi hiyo njema.

Kwa upande wake Mwalimu mkuu wa shule hiyo Mwl. Samwel Sospeter Jonathan, ameshukuru uongozi wa Wizara kwa kuwatembelea Watoto wenye mahitaji maalumu na kuwapatia msaada ambao utawasaidia Watoto kukidhi mahitaji yao muhimu.

''Ugeni huu tumeupokea kwa furaha kubwa kwani umesaidia upatikanaji wa mahitaji ya msingi ya kila siku kwa Watoto hawa ambao wanatoka katika familia duni, tunatoa wito kwa jamii ya Watanzania kuyatambua makundi haya na kuyapa kipaumbele pamoja na kuyatembelea" alisema Mwl. Jonathan.

Alitoa rai kwa wadau mbalimbali nchini kuwezesha upatikanaji wa uhakika wa matibabu kwa Watoto hao kwani shule haina fungu la matibabu hivyo inapata changamoto kuwapatia Watoto huduma za afya pindi wanapougua.

Pia ametoa wito kwa watumishi wa Wizara hiyo kuwa mabalozi wao kwani shule hiyo sio ya kibiashara kwa wadau kusaidia shule hiyo kujenga uzio ili kuimarisha ulinzi na usalama wa Watoto wenye ulemavu wa Ngozi wanaosoma shuleni hapo.

Akizungumza kwa niaba ya wanafunzi wa shule hiyo Monica Isaya anayesokma darasa la saba katika shule hiyo aliwashukuru watumishi wanawake wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuwatembelea na kuwapatia msaada wamefarijika na kuahidi kujitahidi katika masomo yao licha ya ulemavu walionao watafanya vizuri katika masomo yao.

Watumishi hao wamekabidhi vitu mbalimbali ikiwemo taulo za kike, mafuta ya kupikia, sabuni za kufulia, vyakula pamoja na vifaa vya usafi na kuahidi kuwatembelea wakati mwingine.

Shule ya Msingi Buigiri ni ya pekee mkoani Dodoma, ilianzishwa Aprili 30, 1950 kwa sasa ina jumla ya wanafunzi 120 inafundisha Watoto wenye uoni hafifu, wasioona pamoja na wenye ulemavu wa ngozi kuanzia shule ya awali hadi darasa la saba ambapo kwa miaka kumi mfululizo imeshika nafasi ya kwanza Kiwilaya katika matokeo ya darasa la nne na la saba.



# ESTONIA NA UFARANSA KUISAIDIA TANZANIA KUBORESHA MIFUMO YA KODI NA BANDARI.

Serikali ya Estonia imeahidi kuisaidia Tanzania kuboresha mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ya ukusanyaji kodi ili kusaidia kupiga hatua zaidi katika masuala ya usimazi wa kodi na kuongeza uwazi na uwajibikaji.

Ahadi hiyo imetolewa na Naibu Waziri wa Masuala ya Uchumi na Maendeleo wa Estonia, Mhe. Marjin Ratnik, alipofanya mazungumzo na Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), mjini Doha, Qatar, kando ya Mkutano wa Tano wa Umoja wa Mataifa wa nchi zinazoendelea za kipato cha chini unaoendelea nchini humo.

Mhe. Ratnik alisema Serikali yake ipo tayari kuwapokea wataalamu kutoka Tanzania kupata mafunzo ya mifumo ya tehama ya ukusanyaji kodi nchini humo kwa vitendo ili wapate utaalam utakaowasaidia wakati wa utekelezaji wa majukumu yao.

Kwa upande wake Waziri wa Fedha na Mipango Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, amesema Serikali imepokea rasmi mwaliko wa kuwapeleka wataalamu wa Tanzania kupata mafunzo hivyo wameanza maandalizi ya safari hiyo ambapo mwezi Mei mwaka huu wataalam wanaohusika na masuala ya ukusanyaji kodi watakwenda nchini Estonia kujifunza mifumo mbalimbali ya ukusanyaji kodi.

“Juhudi hizi ni utekelezaji wa agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, la kuboresha mifumo ya kodi ili kuwepo na uwazi katika ukusanyaji”, alisema Dkt. Mwigulu.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Wizara ya Fedha na Mipango Zanzibar, Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum, alisema kuwa kuwepo kwa mifumo bora ya ukusanyaji kodi itaongeza uwajibikaji wa watalaam wanaohusika na ukusanyaji kodi.
Aliongeza pia kuwepo kwa mifumo ya pamoja ya ukusanyaji kodi itamsaidia mlipakodi kulipa kodi mara moja katika Taasisi zote zinazohitaji kufanya hivyo.

Katika tukio jingine Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, alikutana na kufanya mazungumzo na Waziri wa Maendeleo na Ushirikiano wa Kimataifa wa Ufaransa, Mhe. Chrysoula Zacharopoulou ambapo Waziri huyo alisema Serikali yake ipo tayari kusaidiana na Tanzania katika ujenzi wa bandari itakayohudumia Tanzania na nchi jirani

“Ufaransa ipo tayari pia kutusaidia kukuza sekta binafsi ambayo imekuwa ikitoa ajira nyingi kwa vijana nchini”, alisema Dkt. Nchemba.
Aliongeza kuwa Serikali ya Ufaransa itaendelea kushirikiana na Tanzania katika kuboresha miundombinu ya barabara, nishati na umeme wa jua ili iweze kutumika katika shughuli za uzajilishaji.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Zanzibar, Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum, alisema kuwa Ufaransa imetangaza rasmi kushirikiana na Tanzania katika kukuza sekta ya utalii kwa kuwa ina mchango katika pato la Taifa.
Aliongeza kuwa Serikali ya Ufaransa imekuwa ikiisaidia Zanzibar katika kuboresha sekta mbalimbali ikiwemo miundombinu, afya na nishati.

Kwa upande wake Waziri wa Maendeleo na Ushirikiano wa Kimataifa wa Ufaransa Mhe. Chrysoula Zacharopoulou, alisema kuwa pamoja na ushirikiano mzuri uliopo kati ya Tanzania na Ufaransa, anaamini kuwa bado kuna mengi zaidi ya kushirikiana kati ya nchi hizo mbili.
Mhe. Zacharopoulou alipongeza msimamo wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwenye masuala ya jinsia na nia ya Tanzania kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Jukwaa la Usawa wa Kizazi (Generation Equality Forum) baadae mwaka huu.



# TANZANIA NA DENMARK KUKABILIANA NA MABADILIKO YA TABIANCHI

Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, amesema kuwa Dermark imekubali kushirikiana na Tanzania katika kupambana na mabadiliko ya tabianchi ambayo yamekua yakiathiri shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Dkt. Nchemba ameyasema hayo mjini Doha nchini Qatar, baada ya kukutana na kufanya mazungumzo na Waziri wa Ushirikiano wa Maendeleo na Sera za Mabadiliko ya Tabianchi wa Serikali ya Kifalme ya Denmark, Mhe. Dan Jorgesen, kando ya Mkutano wa Tano wa Umoja wa Mataifa wa nchi zinazoendelea za kipato cha chini unaoendelea nchini humo.

Alisema nchi hizo mbili zimekubaliana kuzielekeza Taasisi zao kuendelea kushirikiana katika nyanja mbalimbali hususani kukabiliana na mabadiliko hayo ya tabia nchi ili kukuza uchumi. "Licha ya makubaliano yaliyofikiwa katika mkutano huu, tumekua na ushirikiano mzuri na Dernmark ambapo Serikali yetu hupokea fedha nyingi kupitia Taasisi za Denmark ambazo hutumika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo", alisema Dkt. Nchemba.

Alisema kuwa mkutano kati ya nchi hizo mbili ni mwendelezo wa mikutano mbalimbali ambayo imekuwa ikifanyika hivyo mazungumzo ya sasa ni jitihada za kuendelea kuimarisha ushirikiano huo wa kimaendeleo katika sekta mbalimbali.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango-Zanzibar, Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum, alisema kuwa Serikali ya Zanzibar imepata manufaa makubwa katika sekta za kijamii ikiwemo afya, elimu na miundombinu.

Alisema Zanzibar na Tanzania kwa ujumla imeweka mikakati kabambe ya kuhakikisha inatekeleza diplomasia ya kiuchumi na nchi mbalimbali ili kuvutia uwekezaji na kuwaletea wananchi maendeleo, hivyo mikutano inayoendelea na nchi nyingine ni miongoni mwa jitihada za kufanikisha azma hiyo.

Kwa upande wake Waziri wa Ushirikiano wa Maendeleo na Sera za Mabadiliko ya Tabianchi wa Denmark, Mhe. Dan Jorgesen, ameipongeza Tanzania kwa kuendeleza ushirikiano kati ya nchi hizo.

Mhe. Jorgesen amesema kuwa pamoja na upya wa Serikali yake iliyopo madarakani baada ya uchaguzi mkuu wa Novemba 2022, Serikali ya mseto ya Denmark itaendelea kuimarisha ushirikiano na Tanzania katika nyanja mbalimbali za kiuchumi na kijamii.

“Mabadiliko ya Tabianchi ni masuala ambayo yanapaswa kupewa kipaumbele na kila mmoja wetu kutokana na athari zinazoendelea kujitokeza kutokana na changamoto hiyo”, alisema Mhe. Jorgesen.

Aidha, Mhe. Jorgesen alisema Serikali yake inayoongozwa na Waziri Mkuu Mhe. Mette Frederiksen, anao ufahamu mkubwa kuhusu siasa za Bara la Afrika hivyo itasaidia kuongeza ushirikiano kati ya Denmark na Tanzania.



# SERIKALI YAWASILISHA BUNGENI MAPENDEKEZO YA UKOMO WA BAJETI 2023/2024

Serikali imewasilisha bungeni Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/24, ambapo imepanga kukusanya na kutumia jumla ya shilingi trililion 44.3.

Bajeti hiyo inajumuisha shilingi trilioni 29.2 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 15.1 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Akiwasilisha mapendekezo hayo bungeni jijini Dodoma Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb) alisema kiasi hicho ni sawa na ongezeko la asilimia 7.0 ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge ya mwaka wa Fedha 2022/23 ya shilingi trilioni 41.5.

Alisema jumla ya mapato ya ndani yanatarajiwa kuwa shilingi trilioni 31.4, sawa na asilimia 70.7 ya bajeti yote ambapo kati ya mapato hayo, mapato yanayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) yanakadiriwa kuongezeka kwa asilimia 13.0 hadi shilingi trilioni 26.7 kutoka makadirio ya shilingi trilioni 23.7 mwaka 2022/23.

“Misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo inatarajiwa kufikia shilingi trilioni 5.4, sawa na asilimia 12.3 ya bajeti yote”, alisema Dkt. Nchemba.

Dkt. Nchemba alisema Serikali inatarajia kukopa shilingi trilioni 5.4 kutoka soko la ndani ambapo shilingi triioni 3.5 ni kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za Serikali zinazoiva na shilingi trilioni 1.9 kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

Alisema Serikali inatarajia kukopa shilingi trilioni 2.1 kutoka soko la nje kwa masharti ya kibiashara ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya miundombinu.

Kuhusu mgawanyo wa matumizi, Dkt. Nchemba alisema kuwa kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 29.2 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikijumuisha shilingi trilioni 12.8 kwa ajili ya ulipaji wa deni la Serikali na gharama nyingine za Mfuko Mkuu na shilingi trilioni 10.9 kwa ajili ya mishahara ikiwemo upandishaji wa madaraja kwa watumishi na ajira mpya, na shilingi trilioni 6.4 kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC).

"Matumizi ya maendeleo yanatarajiwa kuwa shilingi trilioni 15.1 ambapo kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 11.9 ni fedha za ndani, sawa na asilimia 78.3 ya bajeti ya maendeleo na shilingi trilioni 3.2 ni fedha za nje", aliongeza.

Dkt. Nchemba alisema kuwa ukomo wa fedha za maendeleo upo ndani ya wigo wa kati ya asilimia 30 na 40 ulioanishwa kwenye Mpango Elekezi wa Muda Mrefu (2011/12 – 2025/26) ambapo utengaji wa fedha za maendeleo umezingatia miradi inayoendelea ikiwemo miradi ya kimkakati na ya kielelezo pamoja na utekelezaji wa miradi kupitia utaratibu wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP) ili kuipunguzia Serikali mzigo wa kugharamia miradi ya maendeleo kwa utaratibu uliozoeleka.

"Aidha, bajeti ya matumizi ya kawaida imeongezeka kufuatia kukamilika kwa miradi ya maendeleo hususan kwenye sekta za huduma za jamii ambazo kwa sasa zinahitaji fedha za matumizi ya kawaida kwa ajili ya uendeshaji", alibainisha Dkt. Nchemba.

Alisema katika mwaka 2023/24, Serikali inatarajia kuongeza ukusanyaji wa mapato, ili kugharamia sehemu kubwa ya matumizi yake na kuendelea kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti Namba 11 ya Mwaka 2015 pamoja na sheria nyingine kwa lengo la kubana matumizi na kuelekeza fedha kwenye utekelezaji wa vipaumbele vilivyoainishwa.

Dkt. Nchemba alisema utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24 pamoja na Mfumo na Ukomo na Bajeti ya mwaka 2023/24, unatarajiwa kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati, kuimarisha sekta za uzalishaji ili kutoa mchango zaidi katika ukuaji wa uchumi, kuongeza mapato ya Serikali, fursa za ajira na maendeleo ya watu na nchi kwa ujumla na kuongeza upatikanaji wa huduma bora za kijamii kama vile elimu, afya, maji, barabara n.k.

## MATUKIO KATIKA PICHA



Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb) akiwasilisha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/24, kulia ni Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa na Naibu Spika wa Bunge, Mhe. Mussa Azan Zungu, ukumbi wa Pius Msekwa, bungeni jijini Dodoma.



# DKT. NCHEMBA AKUTANA NA UJUMBE WA MOODY'S

Taasisi ya kimataifa inayojihusisha na kuzifanyia tathimini nchi mbalimbali ili kujua uwezo wake wa kukopesheka katika masoko ya fedha ya Kimataifa, Moody's, imetua nchini kwa ajili ya kufanya tathimini hiyo Tanzania.

Akizungumza wakati akiikaribisha timu ya wataalam kutoka Taasisi hiyo Jijini Dodoma, Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb) amesema kuwa tathimini hiyo ni fursa kwa Tanzania kuweza kuyafikia Masoko ya fedha ya Kimataifa yatakayoiwezesha nchi kupata rasilimali fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ya wananchi.

Amesema kuwa uchumi wa Tanzania unaendelea kuimarika licha ya changamoto za Uviko 19 na Vita vya Ukraine na Urusi lakini pia Taifa limepiga hatua kubwa za kiuchumi, kidiplomasia, haki za binadamu na kisiasa.

Dkt. Mchemba alisema kuwa tathimini huru inayofanywa na Taasisi hiyo maarufu Duniani ya Moody's inaiwezesha Tanzania kuaminiwa na Taasisi za fedha za kimataifa hivyo kuchochea uwekezaji ambao utakuza uchumi wa nchi pamoja na ajira kwa vijana.

Alisema kuwa ujio wa wataalam hao unajibu kiu ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyeagiza nchi ifanyiwe tathimini ili kubaini uwezo wake wa kuyafikia masoko ya fedha ya kimataifa katika kuharakisha maendeleo ya watu.

Moody's inaifanyia tathmini Tanzania kwa njia shirikishi itakayowezesha kutoa taswira halisi ya nchi na hatua ambazo imepiga kiuchumi, kijamii na kisiasa.

## MATUKIO KATIKA PICHA



Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), (kulia), akisalimiana na Kiongozi wa jopo la wataalam waliowasili nchini kufanya tathimini ya uwezo wa Tanzania kukopesheka kwenye masoko ya Kimataifa (credit rating) ya Moody's, Bw. John Walsh, Jijini Dodoma.



# WIZARA YA FEDHA YATOA MAFUNZO KWA WAZABUNI KUTOKA BOTSWANA

Wataalamu kutoka Mamlaka ya Rufaa ya Zabuni ya Ununuzi wa Umma nchini Botswana wameipongeza Tanzania kwa kuwa na mifumo imara ya ununuzi na utatuaji wa migogoro ya ununuzi hatua inayochangia kupata wazabuni na wakandarasi wernye sifa za kutekeleza miradi ya maendeleo.

Hayo yameelezwa jijini Dodoma na Msajili wa Mamlaka ya Zabuni ya Ununuzi wa Umma nchini Botswana, Bw. Geoffrey Gotshega, akiongoza ujumbe walipofanya ziara ya mafunzo Wizara ya Fedha na Mipango kujifunza mambo mbalimbali kuhusu utekelezaji wa sera za ununuzi.

Bw. Gotshega alisema kuwa Mamlaka ya Zabuni ya Ununuzi wa Umma Botswana ni mpya, hivyo wamekuja kujifunza namna ya mfumo wa ununuzi Tanzania ulivyoundwa na unavyofanyakazi.

"Mifumo ya ununuzi ya Tanzania ni madhubuti kwa kuwa kanuni zake ni imara, ununuzi unafanyika kwa uwazi kwa njia ya kielektroniki na malalamiko yanafanyiwa kazi kwa uharaka na kuwezesha miradi kufanyika kwa wakati na kuipunguzia serikali gharama", alisema Bw.Gotshega .

Akielezea kuhusu ziara hiyo Kamishna Msaidizi wa Idara ya Sera ya Ununuzi wa Umma wa Wizara ya Fedha na Mipango, Bw. Alex Haraba, alisema kuwa amewaeleza kuhusu Sera ya ununuzi wa umma inayosimamiwa hiyo na majukumu yake ikiwa ni pamoja na kusimamia, kutekeleza na kushughulikia malalamiko ya ununuzi wa umma ili kuwa na tija katika ununuzi wa umma kwa mwananchi na Taifa kwa ujumla.

Kwa upande wake, Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufaa ya Zabuni za Umma -PPAA, Bw. James Sando, alisema lengo la wataalam hao wa sekta ya uzabuni kuja Tanzania ni kutaka kujifunza na kuangalia jinsi ambavyo Tanzania inafanya kazi ya ununuzi na namna itakavyowasaidia katika utendaji kazi wao kwa sababu wamepitisha sheria yao ya ununuzi hivi karibuni.

"Tanzania tumeanza kutekeleza Sheria ya ununuzi miaka 23 iliyopita na tumekuwa na Mamlaka ya Rufaa, ndio maana wenzetu wamekuja kuangalia namna tunavyoendesha mashauri katika Mamlaka na wamefurahia ujuzi tuliowapa", alisema Bw. Sando.

Bw. Sando aliongeza kuwa pamoja na utekelezaji wa majukumu yao PPAA pia wanashughulikia mashauri ambayo yanatokea katika ununuzi wa umma nchini.

Alisema kuwa mteja aliyeomba zabuni na ana malalamiko ambayo yameanzia mchakato katika ununuzi anaweza kwenda PPAA baada ya kuwa amewasilisha kwa Afisa Masuuli na kama Afisa Masuuli atakuwa ametoa maamuzi ndani ya siku saba na hajaridhika anaweza kwenda kwenye Mamlaka hiyo.

Alieleza kuwa, hata kama mchakato mzima wa ununuzi umekamilika na tuzo imetolewa na mradi umeanza kufanyiwa kazi na mikataba ilisainiwa, Mamlaka inaweza kusikiliza lalamiko  na kutoa ufumbuzi.

Ujumbe huo kutoka Botswana unaendelea na ziara hiyo ya mafunzo ambapo wajumbe hao wametembelea Wizara ya Fedha na Mipango na Mamlaka ya Rufaa ya Zabuni za Umma -PPAA, jijini Dodoma.

## MATUKIO KATIKA PICHA



Mwenyekiti wa Ujumbe wa Wataalamu kutoka Mamlaka ya Zabuni ya Ununuzi wa Umma nchini Botswana, Mhe. Jaji Lebotse Kenneth, akieleza jambo wakati wa mafunzo kwa wataalam wa Mamlaka ya Rufaa ya Zabuni za Umma Botswana (kulia) walipofanya ziara kwenye Ofisi za Mamlaka hayo, Tanzania, jijini Dodoma.



Mwenyekiti wa Ujumbe wa Wataalam kutoka Mamlaka ya Rufaa za Zabuni ya Ununuzi wa Umma nchini Botswana, Mhe. Jaji Lebotse Kenneth, akipeana mkono na Kaimu Mwenyekiti wa Mamlaka ya Rufaa ya Zabuni za Umma -PPAA Wakili Rosan Mbwambo, walipowasili kwenye Ofisi za Mamlaka ya Zabuni ya Ununuzi wa Umma Tanzania (PPAA) jijini Dodoma.




# WAKAZI WA KAGERA KUONDOKANA NA ADHA YA NISHATI YA UMEME BAADA YA AFDB NA AFD KUTOA FEDHA

Wakazi wa Mkoa wa Kagera wanatarajia kuondokana na changamoto ya kukosa umeme wa uhakika baada ya Tanzania na Benki ya Maendeleo ya Afrika-AfDB na Shirika la Maendeleo la Ufaransa kusaini mikataba ya mkopo yenye masharti nafuu ya dola za Marekani milioni 161.47 na euro milioni 110, mtawalia, sawa na shilingi bilioni 647.5 za Tanzania.

Mikataba imesainiwa na Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba kwa upande wa Tanzania, Meneja wa Benki ya Maendeleo ya Afrika nchini Tanzania Dkt. Patricia Laverley na Bi. Celine Robert, Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Maendeleo la Ufaransa-AFD.

Dkt. Nchemba alifafanua kuwa kati ya fedha hizo zilizosainiwa, kiasi cha dola milioni 161.47 sawa na shilingi bilioni 374.9 kimetolewa na Benki ya Maendeleo ya Afrika-AfDB na kiasi cha euro milioni 110 sawa na shilingi za Tanzania bilioni 272.6 kimetolewa na Shirika la Maendeleo la Ufaransa-AFD.

Dkt. Nchemba alifafanua kuwa kati ya fedha hizo zilizosainiwa, kiasi cha dola milioni 161.47 sawa na shilingi bilioni 374.9 kimetolewa na Benki ya Maendeleo ya Afrika-AfDB na kiasi cha euro milioni 110 sawa na shilingi za Tanzania bilioni 272.6 kimetolewa na Shirika la Maendeleo la Ufaransa-AFD.

"Katika kutatua changamoto za nishati ya umeme mkoani Kagera, Serikali iliiomba Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD) kufadhili Mradi wa Umeme wa Maji wa Kakono, ambapo kwa pamoja - AfDB; AFD kwa ushirikiano na Umoja wa Ulaya; na Serikali ya Tanzania zimekubali kufadhili mradi huu wenye thamani ya takribani dola za Marekani milioni 325 sawa na shilingi 750 bilioni" alisema Dkt. Nchemba.

Alisema kuwa Serikali imebakiza kusaini mkataba wa msaada kutoka Umoja wa Ulaya wenye thamani ya euro milioni 35 sawa na shilingi 86.7 bilioni na kuuhamasisha Umoja huo wa Ulaya kuharakisha na kukamilisha maandalizi ya ufadhili huo ili mkataba wake usainiwe ili kufanikisha utekelezaji wa mradi huo.

Dkt. Nchemba alisema kuwa Kanda ya Ziwa ni eneo lenye tija kubwa katika uzalishaji wa madini na samaki wanaouzwa nje, ambapo uhitaji wa nishati ya umeme kwa gharama nafuu na wa uhakika ni muhimu kwa ustawi wa sekta husika lakini kwa muongo mmoja sasa, Kanda ya Ziwa imekuwa na sifa ya matumizi ya mitambo ya kutumia nishati ya dizeli ambayo ni gharama kubwa kuiendesha na kusababisha wakai hao kutokua na umeme wa uhakika na wa kutosha.

"Utekelezaji wa mradi huo utakamilika ndani ya miaka mitano (5) na utahusisha ujenzi wa mtambo wa kufua umeme wa MW 87.8 na kazi nyingine zikiwemo ujenzi wa shule ya msingi na kituo cha afya pamoja na barabara ya lami yenye urefu wa kilomita 28 na hivyo kuboresha hali ya maisha ya jamii ya kanda hiyo. Mradi huu pia unahusisha usambazaji wa umeme na utekelezaji wa mpango wa usimamizi wa mazingira na kijamii" alifafanua Dkt. Nchemba

Kwa upande wake Meneja Mkazi wa Benki ya Maendeleo ya Afrika-AfDB, Dkt. Patricia Larveley, alisema kuwa mradi huo utakapo kamilika unatarajia kuwahudumia wakazi 210,000, viwanda vidogo na vya kati pamoja na migodi ya madini eneo la Kaskazini Magharibi mwa Tanzania kwa kuwa na nishati bora na ya uhakika pamoja na kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa ambayo ina athari kwa mazingira.

“Faida za kiuchumi zitakazotokana na uwepo na kukamilika kwa mradi huo, kutasaidia upatikanaji wa nishati yenye gharama nafuu, kuboreshwa kwa maisha ya wakazi wa Kagera, mambo ambayo yatachangia pia ukuaji wa uchumi imara na shindani wa Taifa” alisema Dkt. Laverley.

Alibainisha kuwa kusainiwa kwa mkataba huo, kumeifanya Benki yake kufikisha kiwango cha misaada na mikopo kilichotolewa kwa Tanzania kufikia dola za Marekani bilioni 2.7 ambapo asilimia 86 ya fedha hizo zimeelekezwa kwenye sekta za nishati, usafirishaji, maji na usafi wa mazingira.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Maendeleo la Ufaransa, Bi. Celine Robert, ufadhili wa fedha zilizotolewa na Serikali ya Ufaransa kupitia Shirika lake utasaidia kuimarisha upatikanaji wa nishati ya umeme si tu kwa Tanzania lakini pia nchi jirani ya Uganda ambapo idadi ya wanufaika inakadiriwa kuwa kati ya watu milioni 3 hadi 4.

“Pamoja na juhudi kubwa zinazofanywa kupata rasilimali fedha takribani dola za Marekani milioni 300, hatua hiyo inaashiria ushirikiano mkubwa uliopo kati ya Tanzania, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Umoja wa Ulaya na Shirika la Maendeleo la Ufaransa” alisema Bi. Celine Robert.

Alisema kuwa kwa upande wa Ufaransa, uhusiano mzuri uliopo kati ya nchi hizo mbili, umewezesha kiwango cha misaada na mikopo kufikia wastani wa euro milioni 150 kila mwaka ambapo mpaka kufikia wakati huu, Ufaransa kupitia Shirika lake, imewekeza zaidi ya euro bilioni 1 sawa na zaidi ya shilingi trilioni 2.5.

Naye Waziri wa nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Zanzibar, aliwashukuru washirika hao wa Maendeleo, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Shirika la Maendeleo la Ufaransa, Umoja wa Ulaya kwa kutoa fedha hizo ambazo zitachangia kuboresha maisha ya wananchi lakini pia kuchochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi katika maeneo ya mradi na Tanzania kwa ujumla.

Hafla ya utiaji saini wa mikataba hiyo imeshuhudiwa pia na viongozi mbalimbali wakiwemo wawakilishi wa nchi na mashirika ya kimataifa, akiwemo Naibu Balozi wa Ufaransa Mhe. Axel Guillon. Mkuu wa Ushirikiano wa Eu nchini Tanzania na Jumuiya ya Afrika Mashariki, Bw. Cedric Merel, ujumbe kutoka Mradi wa Umeme Kakono na TANESCO.



# MAREKANI YAAHIDI KUENDELEA KUSHIRIKIANA NA TANZANIA KWA KASI ZAIDI

MAREKANI imeahidi kuendelea kuiunga mkono Tanzania katika jitihada zake za kuimarisha uchumi wake na maendeleo ya wananchi kwa kutoa fedha na ujuzi mbalimbali pamoja na kuvutia uwekezaji kupitia ubia kati ya sekta ya Umma na Binafsi.

Ahadi hiyo imetolewa na Balozi mpya wa Marekani nchini Tanzania, Mhe. Michael Battle, alipokutana na kufanya mazungumzo na Waziri wa Fedha na Mipango Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, katika Ofisi Ndogo za Wizara hiyo, jijini Dar es Salaam, alipofika kujitambulisha.

Mhe. Battle amepongeza hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali katika kusimamia na kukuza uchumi wa nchi na kuamua kuwekeza kiasi kikubwa cha fedha katika Bajeti yake kwenye sekta za uzalishaji zinazogusa maisha ya watu, kikiwemo kilimo.

"Tunaahidi kuwa Marekani itaendelea kuiunga mkono Serikali ya Kiongozi shupavu ambaye situ kwamba anapigania sana maisha ya watanzania, lakini pia amekuwa mwanadiplomasia anayepigania maendeleo na utangamano wa Afrika" alisema Mhe. Battle.

Mhe. Battle alisema kuwa Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amegusa mioyo ya wamarekani na viongozi wake ndiyo sababu za Makamu wa Rais wa Marekani Mhe. Kamara Harris kupanga ziara ya kuitembelea Tanzania ambapo viongozi hao wawili watafungua fursa zaidi za ushirikiano wa kiuchumi na kijamii.

Kwa upande wake, Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, aliahidi kufikisha ujumbe wa Balozi huyo kwa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na kumwahidi kiongozi huyo kwamba Tanzania iko tayari kutumia fursa za ushirikiano wa nchi hizo mbili kuwahudumia Watanzania.

Aliiomba Marekani kupitia Shirika lake na Maendeleo la Kimataifa (USAID), kuhakikisha kuwa inazipa kipaumbele Asasi zisizo za Kiserikali (AZAKI) katika utekelezaji wa program zake mbalimbali hapa nchini kwa kuzijengea uwezo wa kifedha na kiuendeshaji badala ya kufadhili Taasisi za nje pekee zinazopewa fedha kutekeleza miradi hiyo badala ya kuzinufaisha AZAKI za hapa nchni.

Kuhusu uamuzi wa Serikali wa kuzipa kipaumbele sekta za uzalishaji katika mgao wa fedha za Bajeti, Dkt. Nchemba alisema kuwa sekta hizo ikiwemo kilimo, mifugo, uvuvi, uendelezaji wa wafanyabiashara wadogo (Machinga), utakuza uzalishaji wa mazao, lakini pia kuongeza ajira kwa wananchi hususan vijana.

Naye Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID) Bi. Kate Somvongsiri, alimshukuru Dkt. Nchemba kwa kutoa hoja ya Taasisi za wazawa zikiwemo AZAKI, kupewa kipaumbele katika miradi inayotekelezwa kupitia Shirika lake hapa nchini.

Alisema kuwa utaratibu uliopo hivi sasa ni kwamba asilimia 25 ya rasilimali zinazotumika na Shirika lake katika nchi zinaelekezwa kwenye taasisi za wazawa na kwamba kiwango hicho kitaendelea kuongezeka wakati unapowadia kufanya hivyo lakini lengo ni kufika asilimia 50.

Ushirikiano wa Tanzania na Marekani umetimiza zaidi ya miaka 50 ambapo makubaliano ya kwanza ya kuanzishwa kwa uhusiano huo yalisainiwa mwaka 1968.




# DKT. MWIGULU NCHEMBA ATETA NA KAMISHNA WA BIASHARA KANDA YA AFRIKA WA UINGEREZA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, amesema Tanzania amelishauri Shirika la Kimataifa la Uwekezaji la Uingereza (British International Investment- (BII), kuongeza kiwango cha uwekezaji nchini Tanzania ili kukuza biashara

Dkt. Nchemba ametoa wito huo Jijini London, nchini Uingereza, alipoongoza Ujumbe wa Tanzania uliokutana na Menejimenti ya Shirika hilo, ambalo limewekeza katika baadhi ya miradi nchini hapa.

Alisema Tanzania ina fursa nyingi za uwekezaji katika sekta mbalimbali ikiwemo nishati, kilimo, utalii, madini, viwanda na huduma pamoja na rasimali za asili kama vile gesi na maji kwa ajili ya kuzalishaji wa nishati, ardhi yenye rutuba kwa ajili ya kilimo, madini pamoja na hali ya amani nchini, ambavyo kiujumla vinaweka mazingira ya kuvutia kiuwekezaji.

Dkt. Nchemba ameialika timu ya wataalamu kutoka BII kuitembelee Tanzania na kufanya mazungumzo na taasisi na mashirika mbalimbali pamoja na sekta binafsi ili kuangalia maeneo ya kuweka kwa faida ya pande zote zinazohusika.

Naye Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Zanzibar, Dkt. Juma Malik Akil, alisema kuwa Zanzibar, ikiwa sehemu ya Tanzania, inatekeleza program ya uchumi wa bluu inayohitaji uungwaji mkono wa Taasisi za fedha za Kimataifa na kuiomba Taasisi hiyo kushiriki katika ujenzi wa uchumi wa Zanzibar

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Uingereza la Uwekezaji (BII) Bw. Chris Chijiutomi, aliihakikishia Tanzania kwamba iko tayari kuongeza uwekezaji kwa kushirikiana na Sekta binafsi ikiwa ni sera ya Serikali ya Uingereza ya misingi ya kuanzishwa kwa Shirika hilo.

Alisema kuwa Shirika lake lina mtaji wa zaidi ya dola za kimarekani bilioni 11 lakini imewekeza Tanzania kiasi cha dola za kimarekani milioni 215 pekee hivyo kuitaka Tanzania kuainisha miradi ya kipaumbele ambayo shirika hilo litachambua na kutoa fedha kwa kushirikiana na sekta hiyo binafsi.



# UK EXPOT FINANCE KUSAIDIA UJENZI WA BARABARA NA UKARABATI WA UWANJA WA NDEGE PEMBA

Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, ameishukuru Taasisi ya Uingereza inayohusika na utoaji mikopo ya UK Export Finance (UKEF), kwa kukubali kufadhili ujenzi wa miradi kadhaa ya maendeleo nchini Tanzania ukiwemo mradi wa upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba na ujenzi wa miundombinu ya barabara visiwani humo.

Dkt. Nchemba ametoa pongezi hizo alipokutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mtendaji wa UK Export Finance (UKEF), Bw. Tim Reid, Makao Makuu ya Taasisi hiyo, Jijini London, nchini Uingereza.

Alisema kuwa miradi hiyo, si tu kwamba itachokea shughuli za kiuchumi za visiwa hivyo ukiwemo utalii, bali pia itaboresha Maisha ya wananchi wa Tanzania kwa ujumla.

“Ninaishukuru Serikali ya Uingereza kwa kuamua kutoa fedha za ujenzi wa miradi hiyo ambayo itasaidia kuboresha huduma za usafiri mijini na vijijini, itakuza uchumi, fursa za ajira na kuongeza kasi ya kuyafikia masoko, huduma za kijamii kupitia Sekta ya utalii” alisema Dkt. Nchemba.

Dkt. Nchemba aliiomba taasisi hiyo, kuangalia uwezekano wa kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa kipande cha tano cha reli ya kisasa kinachoanzia Isaka hadi Mwanza chenye urefu wa kilometa 249 na miradi mingine ya kimkakati inayoendelea kutekelezwa na Serikali ili miradi hiyo ikamilike kwa wakati na kuchochea maendeleo ya nchi.

"Mradi huu wa reli ni wa kimkakati na unatarajia kufungua milango ya kibiashara kwa kutuunganisha na nchi jirani za DRC Congo na Burundi, na umekusudiwa kuchochea pia biashara na maendeleo ya watu" alisema Dkt. Nchemba.

Naye, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Zanzibar, Dkt. Juma Malik Akil, alisema kuwa wananchi wa Zanzibar, wanasubiri kwa hamu kuanza kwa ujenzi wa miradi hiyo ya upanuzi wa uwanja wa Ndege wa Pemba na ujenzi wa barabara za Unguja na Pemba, ambazo zitakuza shughuli za utalii na Maisha yao kwa ujumla

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa UK Export Finance (UKEF), Bw. Tim Reid, aliihakikishia Tanzania kupata fedha kwa ajili ya miradi hiyo lakini pia kuendelea kufadhili miradi mingine ya kimkakati itakayowasilishwa na Serikali ikiwemo maji na nishati.

Alisema kuwa hivi karibuni Taasisi hiyo itawaita wadau mbalimbali wakiwemo wawekezaji nchini Uingereza, na kuwaeleza kuhusu fursa zinazopatikana nchini Tanzania ili kuvutia mitaji na teknolojia mbalimbali zitakazo saidia kuongeza uzalishaji hususan katika sekta ya kilimo.

Uk Exporter Finance ni Wakala wa Serikali ya Uingereza inayojihusisha na kusaidia uagizaji na uingizaji wa bidhaa nchini humo kwa kutoa mikopo ya mitaji na kukatia bima bidhaa hizo lakini pia kuhakikisha kuwa zinakuwa na bei shindani kwenye masoko.



# DKT. MWIGULU NCHEMBA ANA KWA ANA NA WAZIRI MKUU MSTAAFU WA AUSTRIA

Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), amewahimiza wawekezaji kutoka Austria na Ujerumani, kuharakisha mchakato wa kuwekeza katika sekta ya ujenzi wa makazi ya kisasa na ya gharama nafuu ili kutatua changamoto ya makazi hususan kwenye taasisi za umma hapa nchini.

Dkt. Nchemba ametoa wito huo alipokutana na kufanya mazungumzo na ujumbe wa wawekezaji kutoka Austria na ujerumani, ukiongozwa na Waziri Mkuu Mstaafu wa 10 wa Austria, Dkt. Alfred Gusenbauer, jijini Dar es Salaam.

Wawekezaji hao wameonesha nia ya kuwekeza kwenye ujenzi wa nyumba zenye gharama nafuu zinazotumia teknolojia ya kisasa na rafiki kwa mazingira, sekta ya misitu, kilimo na kuwezesha upatikanaji wa mitambo inayotumika kupakia na kupakua mizigo bandarini.

Dkt. Nchemba, alisema kuwa kuna uhaba mkubwa wa makazi katika sekta za afya, elimu na makazi binafsi hivyo aliwahimiza wawekezaji hao kukamilisha majadiliano na wataalam wa sekta husika ili kama kutakuwa na maridhiano ya gharama nafuu kwa kuzingatia ubora wa makazi hayo, basi mradi huo uanze kutekelezwa.

Alisema kuwa hivi sasa Serikali iko katika mchakato wa kuandaa Bajeti mpya ya mwaka wa fedha 2023/2024 hivyo kama mradi huo utaanza kutekelezwa kwa kutumia mikakati tofauti ikiwemo kuishirikisha sekta binafsi, serikali itaelekeza fedha zilizopangwa kutumika kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu hiyo kwenye sekta nyingine za huduma za jamii.

Kwa upande wake, Waziri Mkuu Mstaafu wa kumi wa Austria, na Kiongozi wa Ujumbe wa wawekezaji hao, Dkt. Alfred Gusembauer, walisema kuwa wamefurahishwa na mazingira tulivu ya uwekezaji yaliyopo nchini na kwamba wanatarajia kuwekeza kwenye sekta muhimu.

Alisema wanatarajia kuwekeza kwenye ujenzi wa makazi nafuu ya nyumba za walimu, ujenzi wa hospitali hospitali na nyumba za wahudumu wa afya, ujenzi wa makazi biafsi ya watu pamoja na hifadhi ya misitu na kueleza kuwa mkutano kati yao na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba ulikuwa wenye manufaa makubwa.

Mkutano huo ulimshirikisha pia Waziri wa Ardhi,Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dkt. Angelina Mabura, Msajili wa Hazina, Bw. Nehemia Mchechu, Kamishna wa Idara ya Usimamizi wa Madeni Wizara ya Fedha na Mipango, Bw. Japhet Justine na Viongozi wengine kutoka Serikalini.



# BENKI YA DUNIA KUSHIRIKIANA NA TANZANIA KUTEKELEZA PPP

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Bw. Lawrence Mafuru amesema kuwa Serikali inafanya majadiliano ya kimkakati na Benki ya Dunia (WB) namna ya kuiwezesha sekta binafsi kushiriki katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kupitia mpango wa ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, yaani PPP.

Alieleza hayo jijini Dodoma baada ya kukutana na kufanya mazungumzo na ujumbe wa Benki ya Dunia ulioongozwa na Mkurugenzi Mkazi wa Benki hiyo Bw. Nathan Belete, ambapo walijadili namna bora ya utekelezaji wa sheria ya PPP pamoja na uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara nchini. Alisema majadiliano hayo ni utekelezaji wa msisitizo na maelekezo yanayotolewa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa sasa ni wakati wa Sekta Binafsi kushirikiana na Serikali kwa ajili ya kuleta maendeleo ya kiuchumi.

Bw. Mafuru alisema Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amesisitiza kila wakati kuwa pale ambapo Sekta Binafsi inaweza kufanya jambo fulani basi hakuna haja ya kutumia fedha za Serikali, lakini changamoto ilikuwa ni namna na mfumo ambao unaweza kusaidia miradi kufanyika kwa njia ya PPP.

"Wenzetu wa Benki ya Dunia wamekua mstari wa mbele katika kutoa fedha sio tu katika miradi ya kijamii, lakini sasa wanajielekeza zaidi kutoa fedha na misaada ya kitaalam kuhakikisha kwamba eneo hili la PPP sambamba na uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji na biashara nchini yanafanikiwa", alisema Bw. Mafuru.

Alisema kwa sasa Serikali imeanza majadiliano ya awamu ya pili na Benki ya Dunia kuhusu msaada ambao umejielekeza kwenye sekta za miundombinu na sekta zitakazoboresha mazingira ya kufanya biashara nchini.

Aidha, alibainisha kuwa Sheria ya Ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP) inafanyiwa marekebisho ili iweze kuwa shindani, ambayo itaweza kuvutia mitaji ya Sekta Binafsi na hatimaye kiwezesha sekta hiyo kushirikiana na Serikali katika kutekeleza miradi.

Alisema hatua hiyo itaweza kuipunguzia Serikali mzigo wa kibajeti ili fedha ambazo zilipangwa kutumika kwenye miradi ambayo inaweza kufanywa na Sekta Binafsi zielekezwe kwenye sekta za kijamii ambazo haziwezi kuvutia Sekta Binafsi.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkazi wa Benki ya Dunia, Bw. Nathan Belete alisema benki hiyo imeamua kujadiliana na Tanzania kuhusu namna bora ya utekelezaji wa miradi kwa njia Sekta ya Umma na Binafsi (PPP) kwa kuwa ni miongoni mwa vipaumbele vya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Alisema majaliano na Serikali yalikuwa mazuri na anaamini kwamba makubaliano yao yataleta mabaliko katika mfumo wa utekelezaji wa PPP nchini na kuchochea maendeleo ya nchi.

Bw. Belete aliahidi kuendelea kushirikiana na Tanzania kwa karibu katika kutekeleza matarajio ya maendeleo.